**SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA**

__________

**(SURAYA 290)**

______

**SHERIA NDOGO ___**

**Zimetungwa chini ya vifungu vya 7(1) na 16(1) _____**

## SHERIA NDOGO ZA (ADA NA USHURU) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA SONGEA 2018

| | | | |
|---|---|---|---|
| Jina la sheria tarehe ya kuanza kutumika | 1. | | Sheria hizi Ndogo zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru), Halmashauri ya Wilaya ya Songea za mwaka 2018 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa katika gazeti la serikali. |
| Eneo la kutumika | 2. | | Sheria hizi Ndogo zitatumika katika eneo lote la Mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya Songea. |
| Tafsiri | 3. | | Katika Sheria hizi Ndogo tasfiri za maneno zitatumika kama ifuatavyo:- |

‘**Ada'** maana yake ni malipo yatakayolipwa kwa ajili ya huduma na vibali vitolewavyo na Halmashauri.

**‘Ushuru'** Maana yake ni ada au tuzo linalotakiwa kulipwa kwa kupata huduma au kuendesha biashara kwenye eneo la Halmashauri;

**"Afisa Muidhinishwa"**maana yake ni Afisa yeyote wa Halmashauri aliyeteuliwa na Mkurugenzi kusimamia utekelezaji wa sheria ndogo hizi.

**"Halmashauri "**maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Songea.

**"Mkurugenzi"** maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri na ni pamoja na mtumishiwa Halmashauri atakayetekeleza majukumu ya mkurugenzi.

**"Wakala"** maana yake ni mtu au taasisi yoyote iliyoteuliwa na Halmashauri kutekeleza jambo lolote chini ya sheria hizi ndogo kwa niaba ya Halmashauri.

| | | | |
|---|---|---|---|
| Ada ya Ushuru | 4. | (1) | Kutakuwa na ada na ushuru utakaotozwa na Halmashauri kwa huduma na shughuli kama zilivyoonyeshwa kwenye Majedwali ya Sheria Ndogo hizi. |

(2) Ada na Ushuru utakaotozwa chini ya Sheria Ndogo hizi unapaswa kulipwa kabla ya mlipaji kupata huduma inayolipiwa.

(3) Halmshauri itatoa stakabadhi yenye nembo ya Halmashauri kwa ajili ya malipo ya ada na ushuru uliolipwa.

| | | | |
|---|---|---|---|
| Wajibu kulipa ushuru | 5. | (1) | Ni wajibu wa kila mtu anayestahili kulipa ada na ushuru utozwao kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi, kulipa ushuru au ada kama ilivyoelekezwa kwenye majedwali ya Sheria Ndogo hizi. |
| | | (2) | Ni wajibu wa mtu yeyote anayelipa ada na ushuru kudai na kuhakikisha anapewa stakabadhi kwa malipo anayotoa. |
| Msamaha wa kodi | 6. | (1) | Mtu yeyote ambaye atakuwa na shughuli kama inavyoonekana katika majedwali ya sheria ndogo hizi atasamehewa ada na ushuru kama shughuli hiyo itakuwa siya faida, lakini ni lazima shughuli hiyo itambulike kisheria kama ni shughuli isiyo na faida kutokana na usajili au kibali cha taasisi au shughuli ya mtu huyo. |
| Kazi ya afisa Muidhinishwa | 7. | (1) | Afisa Muidhinishwa atakuwa na mamlaka ya kuingia na kufanya ukaguzi kwa shughuli yoyote iliyotajwa na Sheria Ndogo hizi kwa lengo la kuona kama Sheria Ndogo hizi zinafuatwa. |
| Mamlaka ya Mkurugenzi | 8. | (1) | Mkurugenzi au Afisa Muidhinishwa atadai kwa maandishi, madai yoyote ndani ya siku 14 kama ushuru huo au ada hiyo itakuwa haijalipwa na kama mdaiwa hatalipa ndani ya siku hizo, atafunguliwa mashtaka mahakamani. |
| | | (2) | Mkurugenzi au Afisa Mudhinishwa katika muda wowote kabla ya hukumu kutolewa anaweza kufuta shtaka mahakamani iwapo tu mdaiwa atalipa ushuru huo. |
| Uteuzi wa wakala | 9. | | Halmashauri inaweza kumteua kwa maandishi Mtu yeyote ,Taasisi au kampuni kuwa wakala wa kukusanya ada na ushuru kwa ajili ya eneo lote au sehemu ya eneo la Halmashauri. |
| Wajibu wa Wakala | 10. | (1) | Wakala atakayeteuliwa chini ya fungu la 9 la Sheria Ndogo hizi, atawajibika; |

(a) Kutoa taarifa ya maandishi juu ya majina au orodha ya watu wanaotakiwa kutozwa ushuru au ada ndani ya eneo au sehemu ya eneo ambapo ameteuliwa kukusanya ushuru;

(b) Kukusanya na kupokea ada na ushuru kutoka kwa kila mtu anayedaiwa ada na ushuru chini ya Sheria hizi Ndogo;

(c) Kuwasilisha pesa zote alizokusanya kwa Halmashauri kwa mujibu wa mkataba;

(d) Kuwasilisha kwa Halmashauri taarifa ya jina la mtu yeyote atakayeshindwa kulipa kiasi cha deni analodaiwa kwa ajili ya ada au ushuru wowote uliotozwa chini ya Sheria Ndogo hizi.

Makosa kwa Wakala 11. Wakala yeyote aliyeteuliwa atakuwa ametenda kosa chini ya Sheria Ndogo hizi;

(a) atakayeshindwa kuwasilisha Halmashauri kiasi chochote cha pesa za ada au ushuru alizokusanya; au

(b) ambaye kwa kufahamu atamtoza mtu yeyote kiasi cha ada au ushuru zaidi ya kile kilichowekwa chini ya Sheria Ndogo hizi;au

(c) ambaye kwa uzembe au kwa kufahamu atatoa taarifa za uongo kwa mdomo au kwa maandishi juu ya idadi ya walipa ushuru au kiasi cha ada au ushuru alichokusanya au alichopokea;

(d) ambaye kwa makusudi atashindwa kutekeleza wajibu kama wakala chini ya Sheria Ndogo;au

(e) atakuwa ametenda kosa na atachukuliwa hatua za kisheria na Halmashauri.

Makosa/Adhabu 12 (1) Mtu yeyote atakayevunja masharti ya Sheria ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na atashtakiwa mahakamani na akipatikana na hatia atawajibika kulipa faini isiyopungua laki mbili (200,000/=) na isiyozidi Milioni moja au atatumikia kifungo cha miezi isiyopungua miezi kumi na mbili na isiyozidi miezi ishirini na nne jela au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

(2) Pamoja na adhabu atakayopewa mkosaji katika Sheria Ndogo chini ya fungu la 12(1) mkosaji atawajibika kulipa Halmashauri gharama iliyoingia kutokana na kuvunja masharti ya Sheria Ndogo hizi.

Kufifilisha Kosa 13. (1) Mkurugenzi wa Halmashauri anaweza kufifilisha kosa kwa kumtoza mtu au taasisi faini isiyopungua shilingi elfu hamsini (50,000/=) na isiyozidi shilingi Laki Tatu (300,000/=) endapo mtu au taasisi hiyo itakiri kwa maandishi kutenda kosa chini ya sheria Ndogo hizi na kukubali kulipa faini na kiasi cha Ada au Ushuru anachodaiwa.

14.Sheria Ndogo hii inafuta Sheria Ndogo zifuatazo:-

Kufutwa kwa Sheria Ndogo GNNO.182/2014, ya Tarehe 20/06/2014.

(a) Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Wilaya ya Songea, 2014. GN No.182/2014.

**JEDWALI LA KWANZA**

*Limetengenezwa chini ya kifungu cha 4(1)*

**SEHEMU I**

**USHURU WA MIFUGO (MNADANI)**

| AINA YA MFUGO | KIWANGO (BEI YA KUNUNULIA MFUGO) |
|---|---|
| (i) Ngo'mbe | Shilingi 5000/= kwa kila mmoja |
| (ii) Mbuzi/Kondoo | Shilingi 2000/= kwa kila mmoja |
| (iii) Nguruwe | Shilingi 2000/= kwa kila mmoja |
| (iii) Kuku/Kanga/Bata | Shilingi 500/= kwa kila mmoja |

**SEHEMU II**

**ADA/USHURU WA MACHINJIO NA UKAGUZI WA NYAMA**

| Na. | AINA ZA MFUGO | USHURU WA MACHINJIO(Tsh) | ADA YA UKAGUZI WA NYAMA(Tshs.) |
|---|---|---|---|
| 1 | Ngo'mbe/Punda | 2000/=kila mmoja | 2000/=kila mmoja |
| 2 | Mbuzi/ Kondoo | 1000/=kila mmoja | 1000/=kila mmoja |
| 3 | Nguruwe | 1000/= kila mmoja | 1000/= kila mmoja |

**SEHEMU III**

**ADA/USHURU KWA WATOAJI HUDUMA YA TIBA ASILIA NA WAUZAJI WA DAWA ZA JADI**

| Na. | KIBALI KWA MTOA HUDUMA | ADA KWA MWAKA(Tsh.) |
|---|---|---|
| 1 | Waganga wa jadi | 100,000/= |
| 2 | Taasisi yoyote | 100,000/= |
| 3 | Wauzaji wa dawa za asili/kienyeji | 50,000/= |

**SEHEMU IV**
**ADA YA KIBALI CHA BURUDANI**

| Na. | BURUDANI | ADA KWA SIKU(Tsh.) |
|---|---|---|
| 1 | Muziki, Sanaa za maonyesho, ngumi, mazingaombwe n.k | 30,000/= |
| 2 | Ngoma/sherehe nyumbani | 20,000/= |

**SEHEMU IV**

**ADA/USHURU KUEGESHA MAGARI YA NAYOINGIA KATIKA MAGULIO, MASOKO NA MINADA**

| NA. | AINA YA MAGARI | USHURU KWA SIKU (TSH.) |
|---|---|---|
| 1 | Kwa gari/basi kubwa | 2000/= |
| 2 | Kwa Magari madogo(Hiace) | 1,000/= |
| 3 | Kwa Taxi | 1000/= |
| 4 | Pikipiki | 1000/= |
| 5 | Magari binafsi yasiyo ya Biashara | 500/= |
| 6 | Gari dogo la mizigo (Loriau Pick-up chini ya Tani 7) | 2,000/= |
| 7 | Gari kubwa la mizigo zaidi ya Tani7 | 3000/= |

**SEHEMU V**

**USHURU WA MATANGAZO YABIASHARA**

| NA. | AINA YA MATANGAZO | KIWANGO (Tshs) |
|---|---|---|
| 1. | Ada ya maombi ya kuweka kibao au kufanya matangazo | 5,000/= kwa kila tangazo |
| 2. | Matangazo yasiyong'aa kwa kila futimoja ya mraba. | 10,000/= kwa mwaka |
| 3. | Matangazo yanayong'aa kwa kila futi moja ya mraba. | 15,000/= kwa mwaka |
| 4. | Matangazo yenye, au yasiyo na mng'aro yasiyofikia futi moja ya mraba. | 5,000/= kwa mwaka |
| 5. | Matangazo kwa kutumia kipaza sauti | Mtu binafsi 20,000/= kwa siku |
| | | Kampuni/Taasisi100,000/= |

## SEHEMU VI

## ADA/USHURU KATIKA MASOKO NA MAGULIO

| Na. | AINA YA BIASHARA | USHURU KWA SIKU(TSH.) |
|---|---|---|
| 1 | Biashara ya Nguo za mitumba | 1,000/= |
| 2 | Biashara ya nguo za Madukani | 1,000/= |
| 4 | Biashara ya viatu vya mitumba | 1,000/= |
| 5 | Biashara ya mama lishe | 1,000/= |
| 6 | Biashara ya vileo | 1,000/= |
| 7 | Biashara ya kuuza nyama | 5,000/= |
| 8 | Michezo mbalimbali katika soko | 2,000/= |
| 9 | Biashara za bidhaa za urembo | 1,000/= |
| 10 | Biashara ya vyombo vya ndani | 1,000/= |
| 11 | Biashara ya samani mbalimbali | 1,000/= |
| 12 | Biashara nyingine | 1,000/= |

## SEHEMU VII

## ADA/USHURU MAZAO YA MISITU

| Na. | AINA | KIWANGO (Tsh.) |
|---|---|---|
| 1 | Mkaa | 5% ya bei ya shambani |
| 2 | Mbao | 5% ya bei ya shambani |
| 3 | Kuni | 5% ya bei ya shambani |
| 4 | Nguzo | 5% ya bei ya shambani |
| 5 | Gogo | 5% ya bei ya shambani |
| 6 | Fito | 5% ya bei ya shambani |
| 7 | Asali | 5% ya bei ya shambani |
| 8 | Nta | 5% ya bei ya shambani |
| 10 | Kibali cha kukata mti au kuvuna mti | Mti Binafsi1000/= kila mmoja |

**SEHEMUVIII**

**ADA/USHURU MAZAO YA KILIMO**

| **Na.** | **AINAYAZAO** | **KIWANGO (Tsh.)** |
|---|---|---|
| 1 | Mpunga | 3% ya bei shambani |
| 2 | Maharagwe | 3% ya bei shambani |
| 3 | Mahindi | 3% ya bei shambani |
| 4 | Ufuta | 3% ya bei shambani |
| 5 | Matikiti | 3% ya bei shambani |
| 6 | Mtama | 3% ya bei shambani |
| 7 | Mazao mengine | 3% ya bei shambani |

**SEHEMU IX**

**ADA/USHURU WA MADINI YA UJENZI**

| **NA** | **BIDHAA** | **KIWANGO(TSHS)** |
|---|---|---|
| 1 | Maombi ya kibali cha kumiliki eneo la kuchimba madini ya ujenzi | 50,000/= kwa kila kibali kwa eneo chini ya 40,000sq m.<br>300,000/= kwa kila kibalikwa eneo zaidiya 40,000sq m. |
| 2 | Ushuru kwa madini yafuatayo:- | |
| | (a) Tarrazo | 2000/=kwa tani |
| | (b)Mawe | 1500/= kwa tani |
| | (c) Moramu | 1000/= kwa tani |
| | (d) Kokoto | 1000/=kwa tani |
| | (e) Udongo/kifusi | 1000/= kwa tani |
| | (f) Mchanga | 1000/= Kwa tani |
| | (g) Madini mengine yote yanayopatikana ya Halmashauri ya Wilaya ya Songea na kusafirishwa nje ya Halmashauri kama Makaa ya mawe | 1000/= Kwa tani |
| | (h) Madini mengine yote | 1000/= kwa tani |

**SEHEMU X**
**ADA YA USAJILI WA MAGARI**

| Na. | AINAYAGARI | KIWANGO(Tsh.) |
|---|---|---|
| 1 | Taksi | 50,000/= kwa mwaka |
| 2 | Magari y a mizigo | 30,000/= chini ya tani moja na nusu kwa mwaka |
| | | 50,000/= zaidi ya tani moja na nusu kwa mwaka |

**SEHEMU XI**
**ADA YA UKAGUZI WA KIAFYA**

| Na. | AINA | KIWANGOTsh |
|---|---|---|
| 1 | Nyumba za starehe (baa,vilabu vya pombe za kienyeji na nyumba ya kulala wageni | 10,000/= kila baada ya miezi sita |
| 2 | Maduka ya bidhaa | 5,000/= kila baada ya miezi sita |
| 3 | Nyumba za kutengeneza na kuuziwa vyakula na nyama choma | 5,000/= kila baada ya miezi sita |
| 4 | Ukaguzi kwa maombi ya kufungua biashara | 10,000/= |
| 5 | Ukaguzi kwa maombi ya kufungwa biashara baada ya ukaguzi ili kufunguliwa upya | 10,000/= |
| 6 | Ukaguzi wa viwanda vikubwa | 100,000/= kwa mwaka |
| 7 | Ukaguzi wa viwanda vya kati | 50,000/=Kwa mwaka |
| 8 | Ukaguzi wa viwanda vidogo | 20,000/= kwa mwaka |
| 9 | Ukaguzi wa wahudumu wa vyakula | 15,000/= kila baada ya miezisita |

**SEHEMU XII**
**ADA/USHURU MWINGINE**

| Na. | AINA | KIWANGO Tsh |
|---|---|---|
| 1 | Ushuru wa Bima/Kamisheni | 2.5% ya makusanyo |
| 2 | Ushuru wa Mnada wa jumla wa kitu kinachonadiwa | 5% ya bei ya mnada |

| | | |
|---|---|---|
| 3 | Choo cha umma cha kulipia | 200/= |
| 5 | Ushuru wa Huduma (Service levy) | 0.3% ya mapato ya kampuni, mtu binafsi(sole trader) au Taasisi ya kibiashara kwa mwaka baada ya kutoa kodi ya ongezeko la thamani (VAT) |
| 7 | Ushuru wa kulala wageni (Guest House levy) | 20% ya bei ya kitanda kwa usiku mmoja |
| 8 | Ada ya Zabuni | 50,000/= kwa kila moja |
| 9 | Ada ya kukodi ukumbi wa Halmashauri | 200,000/=kwa siku |

**SEHEMU XIII**

**ADA/USHURU WA UJENZI (BUILDING PERMITS)**

| Na. | AINA | KIWANGO Tsh |
|---|---|---|
| **(a) Ada ya Idhini ya Ujenzi** | | |
| (i) | Ghorofa (2 storey and above) | 150,000/= |
| (ii) | Ghorofa moja | 120,000/= |
| (iii) | Nyumba ya biashara (Guest houses, hotels, shopping malls) | 100,000/= |
| (iv) | Kituo cha mafuta | 200,000/= |
| (v) | Nyumba ya makazi na biashara | 70,000/= |
| (vi) | Nyumba za makazi | 30,000/= |
| (vii) | Ofisi binafsi, shule binafsi na hospitali/zahanati binafsi | 100,000/= |
| (viii) | Maghala na Bohari | 200,000/= |
| (ix) | Majengo mengine ambayo hayajatajwa hapo juu | 20,000/= |
| **(b) Adaya mabadiliko (Alteration) ya nyumba/jengo lililopo** | | |
| (i) | Nyumba ya makazi | 10,000/= |
| (ii) | Nyumba ya biashara | 15,000/= |
| (iii) | Ghorofa | 100,000/= |
| (iv) | Kiwanda, bohari, ghala n.k | 100,000/= |

**JEDWALI LA PILI**

**SHERIA NDOGOZA HALMASHAURI YA WILAYAYA SONGEA (ADA NA USHURU) ZA MWAKA 2018**

Mimi………………………….nakiri mbele ya …………………………, Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Songea kwamba mnamo tarehe…… ya mwezi………..mwaka…………..…nilitenda kosa kwa kukiuka masharti ya kifungu cha…………Sheria Ndogo za Halmashauri ya Wilaya ya Songea (Ada na Ushuru) za mwaka 2018. Nipo tayari kulipa kiasi cha ada/ushuru ninaodaiwa pamoja na faini ikiwa Mkurugenzi ataamua kutekeleza mamlaka aliyopewa chiniya Sheria Ndogo zilizotajwa hapo juu

Nathibitisha kwamba maelezo ya hapo juu ni ya kweli nimeyatoa kwa hiari yangu kadri ya ufahamu wangu.

Tarehe…………………………. Sahihi……………………………,,

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Songea ilibandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kwa kufuata azimio lililopitishwa kwenye mkutano wa Halmashauri uliofanyika mnamo Tarehe**……..….**Mwezi**………………**na nembo hiyo ilibandikwa mbele ya:

**……………………….**

**SIMON M. BULENGANIJA**

**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**

**HALMASHAURI YA WILAYA SONGEA**

**……………………………**

**RAJABU H. MTIULA**

**MWENYEKITI**

**HALMASHAURI YA WILAYA SONGEA**

**NAKUBALI;**

**……………………………..**

**SELEMANI S. JAFO. (MB),**

**WN OR-TAMISEMI.**

**DODOMA**

**TAREHE:………………...2018.**